

**HOTUBA YA DR SALIM AHMED SALIM KATIKA MDAHALO KUHUSU  
UMUHIMU WA KATIBA KATIKA MAISHA YA WATANZANIA,  
ALHAMISI TAREHE 17 NOVEMBA 2011, UKUMBI WA MAKUMBUSHO,  
DAR ES SALAAM**

- **Ndugu Mgeni Rasmi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr Ghalib Bilal,**
- **Ndugu viongozi wa dini, vyama vyakimata nasi na serikali,**
- **Ndugu wageni waalikwa na washiriki wote,**
- **Mabibi na Mabwana.**

**SHUKRANI**

**Kwanza kabisa napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wote mliokuja kuungana nasi katika mdahalo huu ambao umeandaliwa na Taasisi ya Mwalimu Nyerere kwa madhumuni ya kuchangia katika juhudi zinazofanywa hivi sasa za kuandaa na hatimaye kukubaliana juu ya katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

**Tunapozungumzia Jamhuri ya Muungano ni muhimu kujikumbusha kuwa huu ni muungano wa mataifa mawili yaliyokuwa huru, yaani Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Na ni Muungano ambao miaka mitatu ijayo tutaadhimisha miaka hamsini.**

## MADHUMUNI

Madhumuni ya mjadala huu kutoa nafasi kwa watanzania mbalimbali wakiwemo viongozi wetu wa vyama vyakisiasa, viongozi wetu wa serikali, vyama vyakiraia, viongozi wa dini, viongozi wa kijamii na wataalamu wetu mbalimbali kutoa maoni yao kuhusiana na zoezi hili muhimu lilopo mbele yetu.

Katika kufanya hivyo changamoto kubwa ni kuhakikisha jinsi ya kulinda na kudumisha misingi mikuu ya utaifa wetu. Misngi hiyo ni pamoja na Utu, Umoja, Demokrasia na Amani ya taifa letu.

## WAKATI MUAFAKA

Zoezi hili la katiba mpya limekuja wakati muafaka ambapo watanzania tunasheherekeea kutimiza miaka hamsini ya uhuru wa Tanzania Bara na miaka michache ijayo tutakuwa tunasheherekeea miaka hamsini ya Mapinduzi ya Zanzibar na kama nilivyosema hapo mwanzo na pia Muungano wetu ambao ndio umeunda taifa la Tanzania.

Ni wajibu wetu kuhakikisha kuwa tunaitumia vizuri nafasi hii adhimu sio tu kutafakari jinsi gani tumeweza kupata mafanikio na kupambana na changamoto mbalimbali katika miaka hamsini ya sasa lakini vilevile kufikiria na kuchanganua ni aina gani ya Tanzania tunayotaka kuijenga katika miaka hamsini ijayo. Na misngi gani itakayotuongoza huko tunapotaka kufikia.

## KATIBA NI SHERIA MAMA

**Ni muhimu kutambua kuwa katiba ni Sheria mama ya watanzania wote. Zoezi la kutunga katiba katika jamii yoyote ile ni zoezi zito ambalo linapaswa kutekelezwa kwa upeo mpana na busara za pekee.**

**Zoezi la kutunga katiba ni jambo kubwa na la kudumu linalopaswa kuchukuliwa kwa mapana yake, umakini mkubwa na kuhusisha watanzania wote.**

**Ni muhimu kutambua kwamba katiba ni yetu sote na kwa maslahi ya sisi sote na vizazi vijavyo.**

## UMUHIMU WA MUAFAKA

**Kwa kuzingatia hali ya kisiasa hivi sasa na huko tuendako, sote hapa tuna jukumu la kuhakikisha kuwa mdahalo wetu unafanyika katika hali ya kidugu na kuelewana yenyе kutawaliwa na nia njema. Katika upeo huo tunaweza kuhitilifiana bila ya kufarakana. Lengo liwe ni kuwezesha makubaliano na sio kuendeleza malumbano.**

**Ni wazi kuwa kila mtu ama kikundi kina maslahi yake katika zoezi hili la kitaifa lakini ni shurti tuwe tayari kuhakikisha kuwa wakati wote tunajenga na kuhakikisha mazingira ya utulivu na busara ambayo yatachangia kutoa nafasi ya makubaliano mionganoni mwetu kwa maslahi ya watanzania wote.**

## **NIA NA MALENGO MEMA**

**Ni vizuri kutambua kuwa hii ni nafasi adimu sana kutokea katika nchi zetu za kiafrika na tunapaswa kuienzi kwa kuhakikisha tunafanikisha zoezi hili kwa mafanikio. Lengo letu liwe ni kujenga zaidi na kuimarisha udugu, mshikamano na maendeleo ya watanzania na sio kubomoa. Lengo liwe kuimarisha mshikamano wetu na isiwe sababu ya kuvunja udugu na mashikamano wa watanzania.**

**Huu ni wakati wetu sote kuonyesha Uzalendo uliotukuka na Uongozi madhubuti katika kuandaa mustakbali mwema zaidi wa Taifa letu.**

**Ndugu mgeni rasmi, Kwa heshima na taadhima sasa napenda kuchukua nafasi kukuomba utufungulie rasmi mdahalo wetu.**

**Asante**